



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2025

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika kidogo. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuendelea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la juu kidogo ya wastani, hali hii ilisababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo iliimarisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa viliripotwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, nyanda za juu Kaskazini mashariki, ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2025

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuendelea kuwa la juu kidogo ya wastani, hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 APRILI, 2025

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):

Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya

mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es

Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua zinazoambatana na

ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua zinazoambatana

na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo

machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):

Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi

vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua

zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz